*Namba ya Upimaji ya Mwanafunzi*..............................

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**
**UPIMAJI WA KITAIFA WA KIDATO CHA PILI**

**021** **KISWAHILI**

**Muda: 2:30** **Mwaka: 2022**

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu A, B na C zenye jumla ya maswali **kumi (10)**.
2. Jibu maswali yote katika sehemu A na B na swali **moja (1)** kutoka sehemu C.
3. Sehemu A na C zina alama **kumi na tano (15)** kila moja na sehemu B ina alama **sabini (70)**.
4. Zingatia maelekezo ya **kila sehemu** na ya **kila swali**.
5. Majibu **yote** yaandikwe kwenye nafasi ulizopewa.
6. Majibu yote yaandikwe kwa kalamu yenye wino wa **bluu** au **mweusi**.
7. Vifaa vyote vya mawasiliano visivyoruhusiwa **havitakiwi** katika chumba cha upimaji.
8. Andika **Namba yako ya Upimaji** katika kila ukurasa sehemu ya juu upande wa kulia.

| KWA MATUMIZI YA MPIMAJI TU | | |
|---|---|---|
| **NAMBA YA SWALI** | **ALAMA** | **SAHIHI YA MPIMAJI** |
| 1 | | |
| 2 | | |
| 3 | | |
| 4 | | |
| 5 | | |
| 6 | | |
| 7 | | |
| 8 | | |
| 9 | | |
| 10 | | |
| **JUMLA** | | |
| **SAHIHI YA MHAKIKI** | | |

2 219021 100011

*Namba ya Upimaji ya Mwanafunzi*..........................

## SEHEMU A (Alama 15)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Katika vipengele (i) hadi (x), chagua herufi ya jibu sahihi kisha andika herufi ya jibu hilo katika kisanduku ulichopewa.

(i) Seti ipi ni sahihi kuhusu vipengele vya fani katika fasihi simulizi?
- A Dhamira, migogoro, mtindo na mafunzo.
- B Ujumbe, matumizi ya lugha, wahusika, mtindo na muundo.
- C Wahusika, matumizi ya lugha, muundo, mtindo na mandhari.
- D Migogoro, ujumbe, wahusika, mafunzo na mtindo.

(ii) Ni muundo upi wa ushairi wa fasihi simulizi unaundwa na mistari/mishororo mitano?
- A Sabilia
- B Takhmisa
- C Tathmisa
- D Tathilitha

(iii) Maendeleo ya Sayansi na Teknolojia yana athari chanya na hasi katika ukuaji wa fasihi simulizi. Zipi ni athari hasi zinazoikabili fasihi simulizi?
- A Hupunguza hadhi na ubora wa kazi za fasihi.
- B Huhifadhi kazi za fasihi simulizi kwa muda mrefu.
- C Huboresha uwasilishaji wa kazi za fasihi simulizi.
- D Hutunza kiini au maana ya ujumbe wa fasihi simulizi.

(iv) Sababu zifuatazo husababisha kutokea kwa utata katika tungo, **isipokuwa**:
- A Neno kuwa na maana zaidi ya moja.
- B Kuzingatia taratibu za uandishi.
- C Kutumia maneno yenye maana ya picha.
- D Kutotamka neno ulilokusudia kwa usahihi.

(v) Juma huimba vizuri <u>sana</u>. Neno linalopigiwa msitari linafanya kazi ya aina ipi ya neno?
- A Kielezi
- B Kivumishi
- C Kitenzi
- D Kihisishi

(vi) Wewe na rafiki yako mmepewa kazi ya kubainisha sentensi yenye vivumishi vya ***a-unganifu*** katika tungo. Je, ni sentensi ipi kati ya zifuatazo itakuwa sahihi?
- A Juma anacheza kwa madoido.
- B Halima mrefu amefika.
- C Abdul na Zuberi wameondoka jana.
- D Janeth wa Dodoma ameingia darasani.

(vii) Kati ya kanuni zifuatazo mojawapo **si** sahihi kuhusu usimulizi wa matukio.

A Kutamka matamshi kwa usahihi.

B Mpangilio mzuri wa mawazo.

C Kujua muundo wa matukio.

D Kutumia lugha kwa usahihi.

(viii) Kati ya alama zifuatazo, alama ipi hutumika badala ya kiunganishi cha kuunga tungo mbili?

A Nucta (.)  B Nukta pacha (:)

B Mkato (,)  D Alama ya mshangao (!)

(ix) Ipi ni dhima sahihi ya kutumia picha na michoro katika kamusi?

A Hufanya kamusi kutambulika kwa haraka.

B Hufanya kamusi kupendwa na wasomaji.

C Hupunguza umakini na idadi ya watumiaji.

D Husaidia wasomaji kuwa na kumbukumbu.

(x) Ipi ni maana sahihi ya shina la neno kati ya zifuatazo?

A Sehemu ya neno yenye mzizi na viambishi awali na tamati.

B Sehemu ya neno yenye mzizi na viambishi awali pekee.

C Sehemu ya neno yenye mzizi na viambishi tamati pekee.

D Sehemu ya neno yenye mzizi na kiambishi tamati vijenzi.

2. Oanisha dhima za nyimbo za fasihi simulizi zilizo katika **Orodha A** na aina za nyimbo kutoka **Orodha B** kisha andika herufi ya jibu sahihi katika kisanduku ulichopewa.

| Orodha A | Orodha B |
|---|---|
| (i) Nyimbo zinazoimbwa ili kuburudisha watu. | A Nyiso |
| (ii) Nyimbo za kuaga mwaka. | B Kimai |
| (iii) Nyimbo zinazoimbwa kwenye maombolezo kama misiba. | C Bembezi |
| (iv) Nyimbo zinazoimbwa kwenye shughuli za kilimo. | D Mbolezi |
| (v) Nyimbo zinazoimbwa kwenye jando na unyago. | E Tumbuizo |
| | F Wawe |
| | G Kongozi |

**Majibu**

| **Orodha A** | (i) | (ii) | (iii) | (iv) | (v) |
|---|---|---|---|---|---|
| **Orodha B** | | | | | |

**SEHEMU B** (**Alama 70**)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

3. Soma kifungu cha habari kifuatacho kisha jibu maswali yanayofuata:

Baba mmoja aliishi na mkewe na mwanae wa pekee wa kike. Baba huyu alikuwa mtu wa kufuata maadili, mila na desturi za kiafrika. Alitamani kila mmoja ndani ya nyumba aishi maisha ya kimalaika. Hakupenda mtu yeyote kwenda kinyume na mawazo yake ili maisha yake yasiende **mrama**, hasa mwanae aliyekuwa **mboni ya jicho lake**.

Binti yule akawa mtoto wa **getikali**, hakuna cha disko wala ufukweni. Mama yake naye hakuruhusiwa kujipamba kiasi cha kupitiliza, ikiwemo kusuka nywele kwa mitindo ya kisasa. Mama na binti yake walilazimika kutii kwa kumuogopa baba yule wa **miraba minne**, mwenye kuongea kwa mrindimo.

Siku moja binti yake aliwaza na kuwazua, akabaini kwamba pale nyumbani hapakuwa na maisha anayoyahitaji, akaamua kufanya uamuzi mbaya wa kutoroka usiku. Baba na mama hawakujua mtoto alikokwenda. Mama akashikwa na **kihoro** akaumwa sana hatimaye umauti ukamfika.

Baba alisikitika sana, akatafakari na kutafakuri, hatimaye akagundua kuwa msimamo wake haukuwa sahihi na kwamba alitakiwa kupokea mawazo na kusikiliza ushauri toka kwa wengine. Vilevile akagundua kuwa hakuna mtu aliyemkamilifu kwani binadamu wote tuna upungufu.

**Maswali**

(a) Pendekeza kichwa cha habari kinachofaa kwa habari uliyosoma kisichozidi maneno matano.

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

(b) Eleza maana ya maneno/vifungu vya maneno vifuatavyo kama vilivyotumika katika habari uliyosoma.

(i) Mrama

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

(ii) Mboni ya jicho lake

(iii) Geti kali

(iv) Miraba minne

(v) Kihoro

(c) (i) Unadhani kwa nini yule binti aliamua kutoroka nyumbani kwao?

(ii) Baba wa familia hii alikuwa na tabia gani?

(d) Andika funzo linalopatikana katika habari hii.

4. Bainisha umbo linalodhihirisha kauli katika maneno yafuatayo kisha taja kauli husika kwa kila neno.

**Mfano**: Anamsomea

(i) Umbo la kauli – e -

(ii) Kauli yenyewe Kauli ya kutendea

(a) Wanapigana

(i) Umbo la kauli……………………………………………………………………………

(ii) Kauli yenyewe……………………………………………………………………………

(b) Atatusomesha

(i) Umbo la kauli……………………………………………………………………………

(ii) Kauli yenyewe……………………………………………………………………………

(c) Limelimwa

(i) Umbo la kauli……………………………………………………………………………

(ii) Kauli yenyewe……………………………………………………………………………

(d) Amechomewa

(i) Umbo la kauli……………………………………………………………………………

(ii) Kauli yenyewe……………………………………………………………………………

(e) Amepigika

(i) Umbo la kauli ……………………………………………………………………………

(ii) Kauli yenyewe……………………………………………………………………………

5. Bainisha viwakilishi katika tungo zifuatazo na kwa kila moja onesha ni kiwakilishi cha aina gani.

**Mfano**: Hili limeoza.

(i) Kiwakilishi - hili.

(ii) Aina - kiwakilishi cha kuonesha.

(a) Yule hapendi ugali.

(i) Kiwakilishi……………………………………………………………………………

(ii) Aina……………………………………………………………………………

(b) Sisi tunapenda kusoma.

(i) Kiwakilishi..........................................................................................

(ii) Aina...................................................................................................

(c) Mtoto wangu amerudi, wako hajarudi.

(i) Kiwakilishi..........................................................................................

(ii) Aina...................................................................................................

(d) Wengi wamepokelewa vizuri.

(i) Kiwakilishi..........................................................................................

(ii) Aina...................................................................................................

(e) Mrefu wa kimo amefika.

(i) Kiwakilishi..........................................................................................

(ii) Aina...................................................................................................

6. Eleza dhima tano za lugha.

(a) ..........................................................................................................

..........................................................................................................

..........................................................................................................

(b) ..........................................................................................................

..........................................................................................................

..........................................................................................................

(c) ..........................................................................................................

..........................................................................................................

..........................................................................................................

(d) ..........................................................................................................

..........................................................................................................

..........................................................................................................

(e) ..........................................................................................................

..........................................................................................................

..........................................................................................................

7. Fafanua sifa tano za misimu katika lugha ya Kiswahili.

(a) ....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

(b) ....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

(c) ....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

(d) ....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

(e) ....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

8. Ni mafunzo gani yanayopatikana katika methali zifuatazo?

(a) Samaki mkunje angali mbichi.

....................................................................................................

....................................................................................................

(b) Mchumia juani hulia kivulini.

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

(c) Akiba haiozi.

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

(d) Safari ni hatua.

....................................................................................................

....................................................................................................

……………………………………………………………………………………………

(e) Akili ni nywele kila mtu ana zake.

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

9. Kazi za fasihi huhifadhiwa kwa njia mbalimbali. Fafanua njia tano za kuhifadhi kazi hizo.

(a) ……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

(b) ……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

(c) ……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

(d) ……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

(e) ……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

**SEHEMU C (Alama 15)**

Jibu swali la **kumi (10)**.

10. Kwa maneno yasiyopungua 150 na yasiyozidi 200, andika insha yenye hoja nne kuhusu Umuhimu wa Michezo.

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

***Namba ya Upimaji ya Mwanafunzi..............................***